

# »Kutengeneza silaji ili kufanikiwa na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa«

Silaji ni malisho ambayo hutengenezwa kutoka kwa mimea yenyeye unyevu mwingi kama vile mahindi bila uingizaji wa hewa ndani ya ghalaa. Silaji huwa tayari baada ya wiki 2–3 za kuhifadhiwa ndani ya ghalaa.

Hata hivyo, ghalaa la shimo linapaswa kuwa na kina cha mita 2.5, upana wa mita 5 na urefu wa mita 12 kwa ajili ya kuongeza uhifadhi wa malisho. Sehemu ya juu ya ghalaa la shimo linapaswa kuinuliwa juu ya ardhi baada ya kulijaza na kulikandamiza. Silaji bora inapaswa kuwa ya kijani, kahawia au rangi ya dhahabu na sio nyeusi.

## Hatua

Kwanza, tandaza lishe ya kijani kibichi katika safu na uikate katika vipande vidogo vya 5–10 cm. Fanyeha kila safu ya lishe iwe na unene wa cm 30–60. Kandamiza kila safu ili kuondoa hewa.

Kisha ongeza molasi au sukari guru kwa kiwango cha 3.5–4.0% ya uzito wa malisho ili kuboresha silaji na ladha yake.

Ongeza nafaka kwenye lishe. Ili kuweka nitrojeni nyunyizia urea kwenye silaji kwa kiwango cha 0.5–1% na ongeza chokaa kwa kiwango cha 0.5 hadi 1% ili kuongeza uzalishaji wa asidi.

Funika sehemu ya juu ya silaji kwa damani ya plastiki, kisha ongeza juu yake udongo wa kina cha inchi 6. Ondoa sehemu ambazo zinaweza kuingiza hewa na maji ili kudhibiti uharibifu wa silaji.

Hatimaye, tumia ghalaa mahsusili ili kutengeneza silaji juu ya

ardhi.